

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA

SHULE YA SEKONDARI BUCHAMBI,  
S.L.P 304,  
**MASWA – SIMIYU.**  
SIMU;  
.....

***Kumb.Na.BUCHSS/ADM/VOL2/01.....***

JINA LA MWANAFUNZI .....  
S.L.P 170, MASWA.

## **YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BUCHAMBI WILAYA YA MASWA MKOA WA SIMIYU MWAKA 2021.**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza (I) katika shule hii mwaka 2021 shule ya sekondari Buchambi ipo katika kata ya Mwamashimba Wilaya ya Maswa.

Muhula wa kuanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 25/01/2021.

### **Mambo muhimu ya kuzingatia**

#### **SARE YA SHULE**

#### **(a) WASICHANA**

- i. Sketi mbili (2) kitambaa cha suti rangi ya bluu bahari (light blue); sketi ziwe za rinda boksi ndefu iguse kisigino cha mguu,
- ii. Shati mbili (2) Tetroni za mikono mifupi; zisishonwe za kubana mwili na ziwe ndefu za kuchomekea wakati wote.
- iii. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika miguu visivyo na urembo wala visigino virefu.
- iv. Soksi nyeupe ndefu jozi mbili (stocking)
- v. Sweta lenye rangi ya sketi (light blue) rangi ya Hijab kwa waislamu ifanane na sare ya shule

**(b) WAVULANA**

Suruali mbili (2) zenye marinda mawili na mifuko mitatu (3) isiyo ya kubandikwa rangi ya bahari (light blue) zisizobana (model)  
Shati mbili (2) tertoni mikono mifupi. Shati itachomekewe ndani ya suruali muda wote  
Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika miguu, visivyo vya urembo.

Soksi dark blue; jozi mbili (2) au nyeusi

Sweta lenye rangi ya suruali; kitambaa kimeambatanishwa kwenye fomu

(c) Sare ya michezo kwa shule hii ni t-shirt rangi nyekundu na tracksut ya blue na viatu vyeusi vya raba jozi moja.

Daftari 15, kalamu na mkebe wa hesabu

Kamusi ya kiingereza kwa kiingereza ni lazima aje nayo.

(d) Wakati unaporipoti lazima uje na nakala ya cheti cha kuzaliwa

**1.0. Sheria na kanuni muhimu za shule hii.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Waziri mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafnuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima

(c) Kushiriki kwa makini kufanya mahudhurio ya jioni (preparation)

(d) Kuwai katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa

(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

(g). Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa

(h). Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na

(i). Kutunza mali za umma

- (g). Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
  - (h). Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
  - (i). Kutunza mali za umma
- 3.2. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.
- (a) Wizi
  - (b) Uasherati na ushoga
  - (c) Ubakaji
  - (d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyo kama vile uvutaji bagi, cocaine, mirungi, kubeli na kadharika.
  - (e) Kupigana au kupiga.
  - (f) Kuharibu kwa makusudi mali za umma.
  - (g) Kudharau Bendera ya Taifa.
  - (h) Kuwa mjamzito/kupata mimba.
  - (i) Kutoa mimba.
  - (j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
  - (k) Kukataa adhabu kwa makusudi.
  - (l) Kuwa na simu ya mkononi
- 2.0. Naambatanisha na fomu zifuatazo;
- 1.1. **Medical Examination Form** ambayo itatakiwa kujazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya serikali. Pia fomu hii aje nayo mwanafunzi siku ya kuripoti shuleni.
  - 1.2. Naambatanisha pia fomu ya historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
  - 1.3. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo yanayotolewa shuleni
- 3.0. **Siku ya kuripoti mwanafunzi aje shuleni na mzazi au mlezi**
- 4.0. **Tafadhari soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

  
.....  
**GODFREY K. G**  
**MKUU WA SHULE**

**HEADMASTER**  
**PRIMARY SCHOOL**  
SWA